

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



05 MEI, 2016



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA TATU – TAREHE 05 MEI, 2016

### I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

#### **WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

#### **WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

#### **MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

## **MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

### **II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

### **III. MASWALI YA KAWAIDA:**

### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **105. MHESHIMIWA ROSE CYPRIAN TWEVE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali imeweka utaratibu wa kuzitaka Halmashauri zote za Wilaya kutenga asilimia 5 ya mapato ili kuwawezesha wanawake na vijana kupata mikopo:-

Je, ni kinamama wangapi au vikundi vya wanawake vingapi vimenufaika na mikopo hiyo katika Halmashauri za Wilaya ya Mufindi, Kilolo, Iringa Mjini na Iringa Vijijini.

## **WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

### **106. MHESHIMIWA FELISTER ALOYCE BURA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Eneo la Msalato lenye kilomita 9 katika ujenzi wa barabara ya Dodoma – Kondoa – Babati kwa kiwango cha lami bado halijakamilika:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa kipande hicho kilichobaki cha Dodoma – Mayamaya.

### **107. MHESHIMIWA DAVID ERNEST SILINDE (MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Ili kurahisisha msukumo wa kimaendeleo na kukuza uchumi katika Bonde la Ziwa Rukwa Serikali iliahidi kujenga daraja linalopita katika Mto Momba kati ya Kata ya Kamsamba (Jimbo la Momba) na Kata ya Kipeta (Jimbo la Kwela) mwaka 2009:-

Je, ni lini ahadi hiyo ya Serikali itatekelezwa?

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:**

### **108. MHESHIMIWA MAKAME MASHAKA FOUM (KIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi:-

- (a) Je, tangu Serikali ilipoanza kutoa mikopo ya Elimu ya juu ni kiasi gani cha fedha kimetolewa mpaka bajeti ya 2015/2016;
- (b) Je, kiasi gani kimerejeshwa ndani ya kipindi hicho;
- (c) Je, chuo gani kinaongoza kwa wanafunzi wake kupata fedha nyingi.

## **WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

### **109. MHESHIMIWA JUMA KOMBO HAMAD (WINGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Serikali imekuwa ikiendeleza zoezi la bomoa bomoa katika maeneo tofauti hapa nchini; zoezi hili limekuwa likiwaathiri Wananchi kiuchumi na hasa kisaikolojia kwa kuwaacha wakiwa hawajui waelekee wapi:-

Je, kwa nini Serikali isiwafidie Wananchi hawa na ukizingatia kwamba wakati wanajenga Serikali ilikuwa inawaona lakini haikuchukua hatua stahiki.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupidisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**DODOMA  
05 MEI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH  
KATIBU WA BUNGE**